ACT
Agricultural Council of Tanzania

Tunaunganisha, Shawishi Na Kutetea

TOLEO Na.47 (JULAI-SEPTEMBA 2023)



# JARIDA LA ACT 2023

## Yaliyomo


- Ziara ya Mafunzo Amberico
- Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Tanzania
- Kongamano la Mifumo ya Chakula Barani Afrika
- ASDP II Mkutano wa Wadau kutathimini Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili
- Ziara ya Mafunzo Ujerumani
- ACT na BAYER Yatanua Wigo wa Mashirikiano
- Wakulima wapatiwa Mafunzo ya Mbinu Bora za Kilimo
- EABC Yaendesha Warsha kwa Wanachama wake
- Warsha ya Uhakiki wa Tafiti


## Tukio Lijalo

Februari 7 - 9, 2024 - Fruit Logistica, Berlin Germany

Oktoba 2, 2023 - Machi 2024 - Dubai Expo, U.A.E

## Habari Muhimu



### Jarida la 2

**Kongamano la Mifumo ya Chakula Barani Afrika**

Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (African Food Systems Forum 2023) lililofanyika Dar es Salaam, Tanzania, liliangazia umuhimu wa Bara Afrika kuimarisha mifumo endelevu ya usalama wa chakula. Jukwaa la mifumo ya chakula ni mkusanyiko wa mawazo chanya, mikakati madhubuti...



### Jarida la 3

**ASDP II Mkutano wa Wadau kutathimini Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili**

Shirika la Pan African Farmers Organization (PAFO), kwa kushirikiana na washirika wake, waliandaa Warsha ya Kikanda kuhusu usimamizi wa maarifa katika utekelezaji wa mradi wa FO4ACP.

## ZIARA YA MAFUNZO AMBERICO

Agosti 5 2023, ujumbe wa watu 15, ukijumuisha wakulima viongozi (Lead Farmers), Maafisa Ugani, na wawakilishi kutoka Sekretarieti ya ACT, walifanya ziara ya mafunzo katika Chama cha Wasindikaji wa Mpunga Mbeya (AMBERICO). Ziara hiyo ya mafunzo ilikuwa na malengo makuu mwaili: Wanufaika wa Mradi wa F04ACP kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu bora za kuendesha kikundi cha kilimo (Farmer Association).



**Wanufaika wa Mradi wa FO4ACP na watumishi wa Baraza la Kilimo wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa ziara AMBERICO**



**Bw. Asafu Aloyce akitoa ufafanuzi kuhusu AMBERICO na kazi zake**

Bwana Asafu alielezea hatua zilizopelekea kuanzishwa kwa chama cha AMBERICO, alibainisha haja iliyokuwepo katika kulinda na kuteta maswalahi ya wakulima wa Mbarali.  AMBERICO ilianzishwa kwa lengo la kulinda maslahi ya wakulima na kutatua changamoto wanakutana nazo katika shughuli zao.  Miongoni mwa mafaniko waliyopata kikundi cha AMBERICO ni pamoja na, msimu wa kilimo uliopita, chama kilifanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwaunganisha wakulima kwa kuwapatia matrekta 78 kutoka Zana Bora Limited, kila moja ikiwa na thamani ya Tsh. milioni 9. Mafanikio haya yaliwezekana kupitia mpango wa mkopo wa miaka miwili. Ziara ya mafunzo iliashiria umuhimu kwa wanufaika wa Mradi FO4ACP, kupata mbinu na mikakati ya kuanzisha chombo kitakacholeta pamoja wakulima. Katika ziara hiyo, wajumbe walishiriki kikamilifu katika majadiliano juu ya mada muhimu, ikiwa ni pamoja na kusimamia utofauti wa uanachama, utatuzi wa migogoro, kupata fedha, na n.k





**Wanafuika wa Mradi wa FO4ACP na watumishi wa Baraza la Kilimo wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa ziara AMBERICO**

## Somo lililopatikana kupitia ziara ya mafunzo

i. Ziara ya AMBERICO inasisitiza umuhimu wa kuwa na sauti ya pamoja na lengo mama la kutekeleza

ii. Njia madhubuti ya kukabiliana na changamoto inaweza kusababisha kuundwa kwa vyama vinavyotumika kama kichocheo cha mabadiliko chanya katika sekta ya kilimo

iii. Uhusiano mzuri na wabi awa maendeleo unaweza kufungua upatikanaji wa rasilimali muhimu

iv. Vyama vinavyoanzishwa vinaweza kuangalia maeneo mbadla ya kutoa huduma kwa wakulima kama vile usindikaji, vifungashio n.k

## Mradi wa FO4ACP

Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) linatekeleza mradi ujilikanao kama ***" Farmer Organization for Africa Caribbean and Pacific – FO4ACP"*** wilayani Mvomero mkoani Morogoro. Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Afrika, Caribbean, na Nchi za Pasifiki (OACPS), na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (IFAD) kupitia Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika (SACAU). Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2019-2023), lengo kuu la mradi kuboresha maisha ya wakulima na kuongeza uzalishaji wenye tija. Mradi ulikusudia kuwafikia wakulima 16,000, mradi umeweza kufikia wakulima 23,000 hadi sasa.

Katika utekelezaji wa mradi kwa mwaka wa mwisho (Desemba, 2023), inatarajiwa wanufaika (wakulima) takriban 24,000 watafikiwa. Wanufaika watapatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora kilimo, matumizi sahihi ya madawa na utunzaji wa fedha. Pia mradi uweza kuboresha mahusiano baina ya wakulima na taasisi za fedha, wauzaji wa pembejeo na wafanyabiashara ya mazao (off-takers)

## MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA TANZANIA

Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo maarufu kama Nane Nane hufanyika kwa wiki moja (kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti), ni tukio la kila mwaka ambalo hutoa fursa ya kuonesha bidhaa zitokanazo na kilimo, vumbuzi na teknolojia mpya kwa maendeleo ya kilimo, na mbinu bora zitakazosaidia kuboresha sekta ya kilimo. Maonesho hayo, huwaleta karibu wakulima, wafanyabiashara, vyama vya wakulima, vyama vya ushirika, taasisi za fedha, Serikali na taasisi zake kwa lengo la kusherehekea na kutambua michango yao katika kukuza na kuchochea uchumi wa taifa. Maonesho ya Kilimo hufanyika katika kanda saba nchini kote yaani; Kanda ya Mashariki (Morogoro), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Magharibi (Tabora), Kanda ya Kusini (Lindi), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), na Kanda ya Ziwa (Mwanza). Maonesho ya Mwakahuu yalipambwa na kaulimbiu isemayo ***"Vijana na Wanawake: Msingi thabiti wa Mifumo ya Chakula Endelevu."***




**Wakulima kutoka Mkindo, Bw. Khaji (Kulia) na Bw. Shebby (Kushoto), wakiwa waelezea wageni walotembelea banda wakati wa monesho ya Nane Nane**

Ngazi ya kitaifa maonesho yalifanyika katika viwanja vya John Mwakangale Mkoani Mbeya na kufunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip I. Mpango. Katika hotuba yake, Makamu wa Rais, aliwahakikishia wadau wa kilimo kuwa Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, kwani mipango hiyo itaongeza fursa za ufadhili na kupunguza gharama za ukopaji.

ACT ilishiriki Nane Nane ngazi ya Kitaifa, sambamba na wadua wengine. ACT ilishiriki sherehe hizo, kwa lengo la kuonesha mchango wake katika kutetea uwepo mazingira wezeshi ya kilimo biashara, na kutoa fursa kwa wakulima kutoka Mkindo na Dakawa kukutana na wadau kama OCP Africa, TFC, Syengeta, Mtenda Kyela Rice Supply, na Raphael Group Limited kwa lengo la kuboresha shughuli zao za kiuchumi. Banda la ACT lilitembelewa na wageni kwa lengo la kufahamu kazi zake, mabadiliko ya kisera, teknolojia za kilimo, na kuboresha mahusiano ya kibiashara na wakulima kutoka Mkindo na Dakawa.

Kimsingi maonesho ya Kimataifa ya Biashara Tanzania kwa mwaka 2023, yalitumika kama sehemu ya kujifunza, kutangaza bunifu katika sekta ya kilimo na kuonyesha shughuli za ushawishi na utetezi zinazofanywa na Baraza la Kilimo.

## KONGAMANO LA MIFUMO YA CHAKULA 2023

AGRF AFRICA FOOD SYSTEMS FORUM

Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika (African Food Systems Forum 2023) lililofanyika Dar es Salaam, Tanzania, liliangazia umuhimu wa Bara Afrika kuimarisha mifumo endelevu ya usalama wa chakula. Jukwaa la mifumo ya chakula ni mkusanyiko wa mawazo chanya, mikakati madhubuti inayolenga kushughulikia changamoto zinazokikabili kilimo Barani Afriaka. Jarida hili la robo mwaka litaangaza Jukwaa la mifumo ya chakula Afrika 2023, kwa kuzingatia umuhimu wake katika fursa za uwekezaji.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2010, AFS imekuwa jukwaa muhimu kwa wadau kutoka sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Wakuu wa Nchi, Mawaziri, Wafanyabiashara, Wabia wa Maendeleo, Wakulima, Vijana, na Wanawake, ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya kilimo Afrika.

## AFS 2023: KUFANYIKA DAR-ES-SALAAM

Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa AGRF 2023, ilitokana na Jukwaa la mwisho lililofanyika mwaka 2012, ambalo lilitoa uthibitisho wa dhamira ya taifa (Tanzania) katika kuleta mabadiliko ya kilimo barani Afrika. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Bi. Vanessa Adams - AGRA, jukwaa la mwaka huu limehudhuliwa na washiriki 5,400 kutoka mataifa 90 duniani ikijumuisha wakuu wan chi watano (5), Wastaafu Wakuu wa Nchi sita (6), makampuni 1200 kutoka sekta binafsi na wawakilishi wa vijana 500. Kwa ufupi, takribani asimili 57 (57%) ya washiriki walikuwa wanawake.

Kauli Mbiu ya Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika 2023 ilikuwa "Rejesha, Zalisha, tekeleza:Suluhisho la Afrika la Maboresho ya Mifumo ya Chakula"ni juhud za pamoja kutatua na kutafsiri maneno hayo kuwa hatua muhimu kupata maboresho ya mifumo ya chakula. Kauli mbiu hii hutumika kama dira ya kimkakati inayoongoza ajenda ya tukio hilo. Inawaweka vijana na wanawake katika mioyo yao kuamsha juhudi za kujenga mifumo ya chakula yenye nguvu sawa, na endelevu.

Dar es salaam ilichaguliwa kuwa mwenyekiti wa Jukwaa hilo kutokana na shughuli za kibiashara na uchumi za kilimo zinazofanyika. Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika lilizinduliwa na Dk. Philipo I. Mpango, Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo alisisitiza dhamira ya Serikali ya Tanzania kuwa na mipango mbalimbali inayolenga kuimarisha ustahimilivu na kubadilisha mifumo ya chakula. Aidha alitajia juhudi hizo ni pamoja na uwekezaji mkubwa katika ufadhili wa kilimo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), ongezeko kubwa la mara nne la bajeti iliyotengwa kwa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, pamoja na utekelezaji wa programu kama Jenga Kesho Yako Iliyobora (BBT-YIA) na Agenda. 10/30.

Programu hizi zimeweka malengo makubwa, mathalani ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030, ikiwiana kikamilifu na kanuni zilizoainishwa katika Azimio la Malabo na Maputo.




Takwimu kwa hisani ya AGRF Sekretarieti



**Makamu wa Rais Dkt. Philipo I. Mpango akifungua Kongamano la Mifumo ya Chakula Barani Afrika, Dar es Salaam.**



**Makamu wa Rais Dkt. Philipo I. Mpango na Rais wa AGRA, Dkt. Agnes Kalibata kwa pamoja wakizindua taarifa ya mwenendo wa kilimo barani Afrika wakati wa mkutano wa AGRF, Dar es Salaam.**

## Jukwaa la Wakulima: Kutafuta njia bora ya kutatua changamoto za Kilimo

Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika mwaka 2023 liliadhimishwa sambamaba na Jukwaa la Wakulima lililofanyika Septemba 8. Jukwaa la Wakulima liliadhimishwa kwa kukutanisha wakulima kutoka mabara tofauti kwa lengo la kuchangia na kupaza sauati juu ya changamoto wanazokabiliana nazo. Hoja kuu ilikuwa ni kutafuta majwabau ya changamoto zao na kubadilishana uzoefu, changamoto, na ubunifu katika mbinu za kilimo. Madak ama vile mbinu endelevu za kilimo, upatikanaji wa rasilimali, fursa za masoko, na nafasi ya teknolojia katika kilimo cha kisasa zilijadiliwa kwa kina.

## AGRF 2023 SAUTI YA VIJANA KWENYE KILIMO

Septemba 7, 2023, vijana walipata nafasi ya kupaza sauti juu masuala yanayowakabili katika sekta ya kilimo. Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihutubia na kushiriki katika mdahalo, uliojumuisha maswali na majibu kutoka kwa vijana. Sambamba na kipengele cha maswali na majibu kutoka kwa Rais Samia, tuzo za vijana maarufu kama Go Gettaz zilitolewa ambapo kwa mwaka huu washindi walitoka Nigeria na Madagaska.

## Mkutano wa Wakuu wa Nchi Katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula:

Tarehe 7 Septemba, Mkutano wa heshima uliwakutanisha viongozi kutoka Bra la Afrika, kujadili namna bora ya kuendeleza mifumo ya chakula. Jarida hili, limeanishabaadhi ya ahadi zilizotolewa na viongozi ni pamoja na;

i. Uwekezaji katika Kilimo: Viongozi wa Afrika waliahidi kuongeza uwekezaji katika kilimo, kutenga sehemu kubwa ya bajeti ya kitaifa kwa sekta hii na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Ufadhili wa kutosha ni muhimu ili kufanya mbinu za kilimo kuwa za kisasa, kuboresha miundombinu na kuimarisha utafiti na maendeleo

ii. Kilimo Kinachostahimili Tabianchi: Kwa kutambua athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo, viongozi wamejitolea kukuza mbinu za kilimo zinazostahimili hali ya hewa. Hii ni pamoja na kupitishwa kwa aina za mazao yanazostahimili ukame, usimamizi bora wa maji, na mbinu endelevu za matumizi ya ardhi.

iii. Kuendelea Kusaidia Wakulima Wadogo: Wakulima wadogo ndio uti wa mgongo wa kilimo barani Afrika. Viongozi hao waliahidi kutoa msaada kwa wakulima hao ikiwa ni pamoja na kupata mikopo, teknolojia za kisasa za kilimo na mafunzo. Kuwawezesha wakulima wadogo ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa chakula na kupunguza umaskini.

iv. Upotevu wa Mazao baada ya Mavuno: Juhudi za kupunguza hasara baada ya kuvuna zilisisitizwa, zikilenga kuboresha miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji, pamoja na upatikanaji bora wa soko, ili kupunguza hasara hizi na kuhakikisha kuwa chakula cha kutosha kinawafikia walaji.

v. Kuimarisha Biashara na Utangamano wa Kikanda: Viongozi wa Afrika walitambua umuhimu wa biashara ya kikanda katika kuhakikisha usalama wa chakula. Waliafikiana kuondoa vizuizi vya biashara na kuboresha miundombinu ya biashara ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa za kilimo kuvuka mipaka.

vi. Kuirisha Mifumo Endelevu ya Chakula: Mkutano huo uliangazia umuhimu wa kukuza mifumo endelevu ya chakula ambayo ni rafiki wa mazingira na yenye uwiano wa lishe. Viongozi wamejitolea kupunguza upotevu wa chakula na kukuza lishe bora.

vii. Uwezeshaji wa Vijana na Wanawake: Viongozi wa Kiafrika walikubali jukumu muhimu la vijana na wanawake katika kuwawezesha kwenye kilimo. Waliahidi kutoa fursa kwa vijana na wanawake katika sekta ya kilimo, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ardhi na rasilimali










**Picha kwa hisani ya AGRF Sekretariet/ Wizara ya Kilimo-Tanzania**

## ASDP II MKUTANO WA MAPITIO YA MASHAURIANO NA WADAU

Tarehe 15 Agosti, 2023, taaisi ya AGRA, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, waliendesha kikao cha nusu siku cha mashauriano na wadau kuashiria kuanzishwa kwa Mapitio ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II - Mid term Review). Lengo kuu la mkutano huu wa mashauriano lilikuwa kutoa taarifa ya utekelezaji, kuangazia changamoto zilizojitokeza, na kuonyesha hatua muhimu zilizofikiwa katika miaka mitano ya mwanzo ya utekelezaji wa ASDP II. Aidha mkutano huo, ulitumika kama jukwaa la kukusanya maoni kutoka kwa wadau amabyo ni muhimu katika zoezi la kufanya tahmini ya utekelezaji wa  Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili.



**wadau wa Sekta Binafsi wakiwa kwenye picha ya pamoja wakatai wa kufanya tathmini ya ADP II**

Mkuatano huo ulikutanisha washiriki kutoka sekta ya umma na binafsi. Wizara na mashirika muhimu kutoka sekta ya umma, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Fedha, na taasisi zake, yalishiriki kikamilifu. Kwa upande wa sekta binafsi, mashirika yenye mchango mkubwa kwenye sekta ya kilimo kama vile ACT, ANSAF, TAHA, SAGCOT na TPSF yalikuwa sehemu ya mjadala huo, huku ACT ikiwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa.

Katika Mkutano huo, Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshugulika na masuala ya Sera, Bunge na uratibu, alisisitiza dhamira ya Serikali katika kusimamia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili



## ZIARA YA MAFUNZO UJERUMANI

Agosti 20 hadi 28, 2023, Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU), kwa kushirikiana na taasisi ya Andreas Hermes Akademie (AHA-International), waliendesha ziara ya mafunzo kwa washiriki wa Program ya Vijana (YLIP) nchini Ujerumani. Lengo kuu la ziara hiyo, lilikuwa ni kuwajengea uwezo vijana kutoka mashirika ya wakulima (Farmer Organizations) barani Afrika ambayo ni wanachama wa SACAU kujifunza namna nchi zilizoendelea zinavyoendesha shughuli za kilimo. Washiriki wa program ya vijana YLIP walipata fursa ya kutembelea maeneo kadhaa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujifunza;




**Washiriki wa Programu ya YLIP kutoka Tanzania wakiwa na Rais wa SACAU Dr. Sinare Y. Sinare (wa tatu kulia) na Makamu wa Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Tanzani Mh. Jitu Soni (w pili kulia)**

Katika mkutano huo, mjadala mkubwa ulijikita katika utekelzaji wa ASDP II kuonekana ni kusuasua. Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) umelenga kuchochea ukuwaji wa kilimo nchini. Maeneo makuu ya ASDP II ni; usimamizi endelevu wa matumizi ya rasimali maji na ardhi, uzalishaji wa tija, uongezaji wa thamani katika bidhaa za kilimo na mazingira wezeshi ya kilimo biashara. Utekelezaji wa haraka wa ASDP II utachochea kwa haraka mageuzi yanayotarajiwa katikaukuaji wa sekta ya kilimo.

Ziara ya kwanza ilihusisha Wizara ya Kilimo ya Ujerumani (German Ministry of Agriculture), ambapo walijifunza kuhusu hatua mahususi zinazochukuliwa na nchi katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Wizara ya Kilimo ya Ujerumani, ilitanabaisha umuhimu kutambua wakulima wadogo na kubadili mtazamo juu yao kwani wanamchango mkubwa katika ustawi wa sekta ya kilimo. Pia waliangazia umuhimu wa vijana kushiriki katika kilimo na vyama vya kilimo kuwa mstari wa mbele kuchochea sera rafiki kwa ustawi wa shughili zao.

Ziara ya pili ilihusisha Taasisi ya Maendeleo Endelevu ya Ujerumani (German Institute of Development and Sustainability), ambapo walijifunza umuhimu wa tafiti na maendeleo katika kilimo (Research and Development). Washiriki pia, walijadili changamoto zinazohusiana na tafiti kama vile; mapendekezo ya tafiti kuwafikia wakulima kwa urahisi (Research Recommendations), na njia bora za kuwasilisha matokeo ya tafiti kwa wadau (Research Findings). Ziara ya tatu ilihusisha kutembelea Tume ya Umoja wa Ulaya (European Commission), ambapo walijifunza faida za soko la pamoja (common market) kwa nchi wanachama. Mfumo wa soko la pamoja unakuza biashara nchi wanachama kwa kuzingatia ubora wa bidhaa ubora, kutengeneza mazingira wezeshi kwa wazalishaji wa ndani kukuza biashara zao kulingana na mahitaji ya soko.




**Washiriki wa Programu ya YLIP wakiwa kwenye picha ya pamoja, Afrika Kusini**

Mwisho washiriki walipata nafasi ya kutembelea Baraza la Wakulima Vijana Ulaya (European Council of Young Farmers) na Umoja wa Mataifa (United Nations). Baraza la Wakulima Viajana lengo lake kuu ni kutetea maslahi ya wakulima vijana na kushughulikia changamoto kama vile upatikanaji wa ardhi, mikopo, na kukabiliana na changamoto ya afya ya akili kwa ustawi se sekta ya kilimo. Katika ofisi za Umoja wa Mataifa, walijifunza juhudi za kukabiliana na kuenea kwa jangwa na njia mbadala za kupambana na mabadiliko makubwa ya kidunia. Kwa ufupi, washiriki walipata fursa ya kujifunza mbinu za kuanzisha mitandao, kuchunguza mitazamo mbalimbali, na kujikita katika tamaduni na mbinu mpya kwenye sekta ya kilimo. Uzoefu huu bila shaka utachangia kwa kiasi kikubwa katika mustakabali wa kilimo, hasa Tanzania na Afrika nzima kwa ujumla.

## ACT NA BAYER YATANUA WIGO WA MASHIRIKIANO

Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) linatekeleza mradi wa mashamba darasa (Demonstartion project) katika mnyororo wa thamani wa zao la mahindi. Mradi huu ni ubia kati ya ACT na Kampuni ya kimataifa ya Bayer Ag, watengenezaji na wasambazaji wa mbegu na viuatilifu. Mradi ulianza kutekelezwa katika msimu wa kilimo wa 2022/23, ushirikiano huo umejikita zaidi katika kuhamasisha matumizi ya pembejeo bora za kilimo katika Wilaya 17 za Tanzania Bara (Wanging'ombe DC, Ludewa DC, Songea DC, Mbinga DC, Hai, Siha, Monduli, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Moshi, Babati, Kiteto, Kondoa, Kilindi, Handeni, Sengerema, Buchosa na Geita) unaolenga kuwafikia wakulima wadogo wapatao 90,300 kwa kuwapa mbinu bora za kilimo na utunzaji wa fedha. Mradi huu wa mashamba darasa ni matokeo ya utekelezaji mzuri wa mradi "Better Farm, Better Livess – BFBL", uliohitimishwa Julai 2021 kwa mafanikio makubwa ya kuwafikia wakulima wadogo takribani 115,000 katika wilaya 29. Kupitia mradi huu, wakulima viongozi, wakala wa pembejeo, maafisa ugani na wafanyabiashra watafikiwa katika wilaya 17.

Kuanzia Septemba 16 hadi 25, timu kutoka Baraza la Kilimo ikiongozwa na Bw. Khalid Ngassa ilifanya ziara katika wilaya za Sengerema, Geita na Buchosa ambapo ilikutana na Maafisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (DALDOs), Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya (DEDs) na wakulima viongozi. Ziara hiyo, ililenga kutambulisha mradi kwa wilaya husika na kutengeneza mifumo ya ufatiliaji na tathmini. Aidha, katika kila wilaya, afisa mazao aliteuliwa kusimamia na kuwezesha uratibu na utekelezaji wa mradi katika ngazi ya wilaya. Kupitia mradi huu, ACT inajukumu la upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa jumla wa shughuli za mradi na kuwezesha wadau wa kimkakati kutimiza wajibu na majukumu yao. Kampuni ya Bayer inatoa ufadhili, mbegu za mahindi na pembejeo nyingine, na msaada wa kiufundi.

## WAKULIMA WAPATIWA MAFUNZO YA MBINU BORA ZA KILIMO

Februari 16 hadi 27 Septemba 2023, ACT iliendesha mafunzo ya Kanuni Bora za Kilimo na matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima viongozi, wakulima, wakala wa pembejeo, maofisa ugani wa kata na wakuu wa idara za kilimo katika wilaya za Sengerema, Buchosa na Geita. Ujumbe kutoka ACT, ulijumuisha maafisa mafunzo wawili, Bw. Khalid Ngassa na Bw. Obed Abraham, pamoja na Mratibu wa Mradi kanda ya ziwa Bw. Leonard Chacha (Sengerema, Buchosa, na Geita), ambao waliendesha mafunzo hayo. Mafunzo ya mbinu bora za kilimo yalisaidia kuimarisha huduma za ugani kwa kufikia idadi kubwa ya wakulima kupitia wakulima viongozi na maafisa ugani waliojengewa uwezo ambao wataendesha mafunzo kwa wakulima wengine (peer farmers). Mafunzo yalifungliwa na Bw. Khalid Ngassa (Meneja Huduma za Uanachama) na Bw. Obed Abraham (Afisa Miradi) ambaye alitoa  maelezo ya jumla ya mradi wa Bayer Ag kwa kutengeneza uhitaji wa bidhaa  BAYER hususan mbegu za DEKALB. Na viuatilifu kama vile BELT, Round Up n.k.




**Washiriki wa mafunzoya Mbinu bora za kilimo wakiwa kwenye picha ya pamoja- Sengrema**



Maafisa ugani wakipokea mbegu za DK kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Mashamba Darasa- Buchosa



Washiriki wa mafunzoya Mbinu bora za kilimo wakiwa kwenye picha ya pamoja- Geita

Kwa ufupi, mafunzo ya mbinu bora za kilimo yaliandaliwa kimkakati kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya pembejeo bora na viuatilifu katika wilaya za Sengerema, Buchosa na Geita. Lengo hili litafikiwa kupitia mafunzo yalitolewa kwa wakulima viongozi, wakala wa pembejeo, maafisa ugani kutoka kila kata ambao watawezesha wadau wengine kufata kanuni za mbinu bora za Kilimo. Mafunzo ya mbinu bora za kilimo yaliangazia maeneo yafuatayo;

i.) Kuandaa shamba,

ii.) Uchaguzi na upandaji sahihi

iii.) Matumizi sahihi ya mbolea,

iv.) Matumizi salama na sahihi ya viuatilifu

v.) Usimamizi wa upotevu wa mazao baada ya mavuno.

Takribani washiriki 150 walihudhuria mafunzo, ni sawa na asilimia mia moja (100%) ya washiriki walinufaika na mafunzo.

## EABC YAENDESHA WARSHA KWA WANACHAMA WAKE

Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC) kwakushirikiana na wabia wake kama Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki (EAGC), Shirikisho la Wakulima wa Afrika Mashariki (EAFF), na Vyama Mwamvuli vya Sekta Binafsi, waliandaa warsha maalumu ya kujengeana uwezo. Mafunzo yalifanyika Julai 24, 2023 Kampala kupitia mradi wa ***"Kuimarisha Ushindani wa Sekta ya Kilimo na Kukabiliana na Machafuko kwa Lengo la Kuboresha Usalama wa Chakula katika Ukanda wa Afrika Mashariki''.*** Warsha hiyo ilikutanisha washiriki kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi ambao wanajishughulisha na masuala ya mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo, uwakilishi huo ulihusisha mashirika kama ACT, TCCIA na mengine. Jumla ya washiriki 25 walikutana katika warsha hiyo, wakiunganishwa na lengo moja la kuwaongezea uwezo na ujuzi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusiana na taratibu za kuuza bidhaa nje na kilimo cha mkataba. Lengo kuu lilikuwa ni kuimarisha ushindani wa sekta ya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula katika ukanda wa Afrika Mashariki, hasa katika kukabiliana na changamoto zilizopo.



**Washiriki wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa Mafunzo, Kampala- Uganda**

## Mafunzo yaliangazia masuala yafuatayo:

Kilimo cha Mkataba: kipengele hiki, kilisisitiza umuhimu wa kilimo cha mkataba katika kuimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo, kuongeza tija, na kukuza ushirikiano endelevu. Aidha, masuala kama vile upatikanaji wa soko, athari zinazoweza kujitokeza na uelewa mpana wa kanuni na taratibu za kilimo cha mkataba. Washiriki, wakiwemo wakulima, wasindikaji na wanunuzi, waliwezeshwa kushiriki kikamilifu katika kilimo cha mkataba, kujadili mikataba yenye usawa, na kusimamia udhibiti wa ubora na utatuzi wa migogoro.

Taratibu za Usafirishaji bidhaa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki: Washiriki walielekezwa taratibu za kufuata wakati wa usafirishaji wa bidhaa ndani ya jumuiya ya Afrika Mashariki, hasa kwa bidhaa za chakula. Pia, mafunzo yalijikita katika kanuni zinazosimamia mauzo ya chakula nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na kuwapa washiriki mbinu za kufikia soko kwa urahisi kwa kuzingatia ubora na mahitaji.

Kwa ufupi, mafunzo yalikuwa na matokeo makubwa sambamba na kutolewa ithibati kwa maafisa 25 kutoka vyama Vyama Mwamvuli vya kilimo kama wabobezi katika fani hiyo. Washiriki waliongeza ujuzi hasa kuhusu taratibu na kanuni za kilimo cha mkataba ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baraza la Kilimo Tanzania liliwakilishwa na Bi Avelina Bernard.

# WARSHA YA UHAKIKI WA TAFITI

Agosti 6, 2023, Baraza la Kilimo Tanzania, kwa ufadhili wa Andreas Hermes Akademie (AHA-International) kupitia Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU), iliendesha warsha ya wadau kujadili matokea ya tafiti kuhusu Ushirikishwaji wa Vyama vya Wakulima katika Sera na Mipango ya Serikali katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; na ilifanyika jijini Mbeya katika ukumbi wa hotel ya Mdope. Lengo kuu la warsha hii, ilikuwa kujadili matokeo ya tafiti kuhusu ***Ushirikishwaji wa Vyama vya Wakulima katika Sera na Mipango ya Serikali katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.*** Warsha hii, ni mwendelezo wa warsha ya kikanda kujadili mabadiliko ya tabianchi iliyofanyika mwezi Julai mjini Johannesburg, ambapo wanachama wa SACAU kutoka nchi 12 walipata fursa ya kuwasilisha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mpango huo wa kitaifa. Warsha hiyo ilikutanisha washiriki 50 ikijumuisha wakulima, wawakilishi kutoka Wizara ya Kilimo, mwakilishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (dawati la mabadiliko ya tabia ya nchi) na wawakilishi kutoka vyama vya sekta binafsi.




**Washiriki wakichangia hoja wakati wa wasilisho la utafiti Mbeya**

Kwa ufupi, warsha ilijadili kwa kina umuhimu wa Serikali katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo kwa kuandaa sera rafiki zinazochochea kilimo endelevu. Pia, washiriki wa warsha walijadili umuhimu wa vyama vya wakulima (National Farmer Organization) kama ACT katika kusaidia wakulima wadogo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na namna teknolojia inaweza kusaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa ufupi, warsha ililenga kujadili mipango ya Serikali na utoaji wa huduma za ugani zilizoboreshwa na kuhakikisha miongozo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inawafikia wakulima vijijini.

# WARSHA YA KUUNGANISHA WAKULIMA NA MASOKO

Agosti 3 na 4 2023, Baraza la Kilimo Tanzania, kwa ufadhili wa Shirikisho la Vyama va Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) kupitia mradi wa FO4ACP; iliendesha warsha ya siku mbili iliyohusu **"mbinu za kufikia soko"** kwa wakulima wa wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro kutoka skimu ya umwagiliaji za Mkindo na Dakawa. Warsha hiyo ililenga kuongeza uelewa na kuongeza uwezo kwa wakulima viongozi (Lead Farmers) na maafisa ugani katika kufikia soko la bidhaa kupitia vyama vya wakulima. Wakulima ambao wanalima kilimo cha teknolojia ya shadidi (System of Rice Intesification) walipatiwa mafunzo ya kina ikiwemo kufikia masoko yenye faida kubwa, kupunguza gharama za miamala, na kuimarisha uwezo wa kufanya mazungumzo ya kibiashara.



Washiriki wa warsha wakiwa kwenye picha Mkindo

Jumla ya washiriki 75 walihudhuria mafunzo hayo ikijumuisha, wakulima viongozi na wakala wa pembejeo (35 kutoka Dakawa na 34 kutoka Mkindo), pamoja na maafisa ugani 3 kutoka kila kijiji. Mafunzo yaliangazia masuala muhimu yanahusiana na zao la mpunga na masoko na mikakati madhubuti yenye lengo la kuwawezesha wakulima wadogo kuchangamkia fursa za kibiashara zinazoibuka.

Kwa ufupi, mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea washiriki maarifa ya kufikia masoko ya bidhaa kwa lengo kuongeza pato na kupambana na umaskini. Warsha hii ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP (2019-2023) unaofadhiliwa na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) unaolengo kuongeza pato la mkulima. Warsha iliendeshwa na Bw. Obed Abraham, Bw. Khalid Ngassa kutoka Sekretarieti ya ACT, na Bw. Hoziel Foya - mwakilishi wa ACT Mvomero.

# MAFUNZO YA MAHUSIANO YA KIFEDHA

Agosti 1 na 2 2023, Baraza la Kilimo Tanzania liliendesha warsha ya siku mbili iliyohusu "Mahusiano ya kibiashara" kwa wakulima wa wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro kutoka skimu za umwagiliaji za Mkindo na Dakawa. Warsha hiyo ililenga kuboresha mahusiano ya kibiashara baina ya wasindikaji na wakulima wadogo. Washiriki 96walishiriki mafunzo ambao ni; wanawake 38, vijana 26, wakulima 69, wafanyabiashara 8, na maofisa ugani 6 kutoka Mkindo na Dakawa.



**Kiongozi wa wakulima (Mr Mwamtobe) akielezea kuhusiana na uzalishaji wa mchele ambao wasindikaji/wanunuzi wa mazao wanahitaji katika kikao kazi Dakawa.**



**Wilmar Meneja Mauzo, Mr Nuruel akizungumza kwa ufupi kuhusiana na ubora wa mchele ambao unahitajika na Kampuni Katika Kijiji cha Dakawa**

Kupitia warsha hiyo, washiriki waliweza kujadilia kwa kina masuala yanayohusiana na bei, taratibu za malipo, masharti ya bidhaa na masuala ambayo yanaweza kuchochea mazingira ya biashara yenye faida baina ya wakulima na makampuni yanayonunua bidhaa. Warsha hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP (2019-2023) unaofadhiliwa na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) unaolengo kuongeza pato la mkulima. Warsha iliendeshwa na Bw. Obed Abraham, Bw. Khalid Ngassa kutoka Sekretarieti ya ACT, na Bw. Hoziel Foya - mwakilishi wa ACT Mvomero.

## Dira na Dhamira

### MISSION

Kuwa na sekta ya kilimo iliofanikiwa, endelevu na shindani inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na msukumo wa kisekta binafsi.

### VISION

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara

## Bodi ya Uhariri

- Bw. Timoth Mmbaga – Mwenyekiti
- Bw. Mark Magila - Mjumbe
- Bw. Khalid Ngassa - Mjumbe

## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130, Dar es Salaam

Simu: (+255) 719260726
Barua pepe: act@actanzania.or.tz
Tovuti: www.actanzania.or.tz

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka kwa wanachama na wadau wengine zinazohusu ustawi wa sekta ya kilimo nchini
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za sekta ya umma na binafsi katika uenddelezaji wa kilimo-biashara

## Hii Ndiyo PFS

Ubia wa mradi wa PFS unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania. Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP2) katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo-biashara na uwekezaji.

### Malengo ya Mradi

Lengo kuu ni; Kuongeza usalama wa chakula na lishe, nakupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu walishe kwa Watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la kilimo Tanzania (ACT). Utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unahimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafanikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha asasi za kiraia 35, wabia kutoka sekta ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakao shirikishwa katika kazi ya ubia.

### Akaunti za Mitandao ya Kijamii:

LinkedIn @barazalakilimo
Twitter @act_tz
Instagram barazalakilimotanzania
Facebook Agricultural Council of Tanzania

**PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenziwa ACT**